TANGAZO LA SERIKALI Na. 307 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MTERA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Mtera ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mipangokina ya eneo

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

*Tangazo la Serikali Na.307 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira - nukta 808394MS, 9210769KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 1.16 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira - nukta 809139MS, 9209853KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Mashariki kwa umbali wa kilomita1.08 kwa kufuata korongo hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira - nukta 809682MS,9209005KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 5.0 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenye majira - nukta 805304MS, 9206386KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.56 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P5 yenye majira - nukta 804834MS, 9207719KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira - nukta 803782MS, 9209148KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 4.8 hadi ulipoanzia’’

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*